**SEHEMU YA C: RIWAYA**

**Jibu swali la 4 au 5**

**Kidagaa kimemwozea: Ken Walibora**

4. “Ni kosa letu sisi sote... kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kumpa uwezo wa kutekeleza ukatili wake.”
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Kwa kurejelea wahusika wanne, thibitisha kwamba matatizo yanayomkumba mwafrika ni msiba wa kujitakia. (alama 16)

5. Mwanamke ametwezwa na pia ametwazwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea riwayanzima. (alama 20)

**SEHEMUYA C: HADITHI FUPI**

**Ken Walibora na S. A Mohammed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

6. Masaibu ya vijana ni suala ambalo limeshughulikiwa kwa kina katika diwani ya Damu Nyeusi na hadithi nyingine. Thibitisha kauli hii ukirejelea. Samaki wa Nchi za Joto, kanda la Usufi, Shaka ya Mambo, Ndoa ya Samani na Tazamana na Mauti. (alama 20)

7. a) Jadili maudhui yoyote manne katika hadithi fupi ya Maeko. (alama 16)
   b) Eleza sifa nne za Duni (alama 4)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. a) Taja sifa za tanzu, zifuatazo za fasihi simulizi. (alama 6)
      i) Mivigha
      ii) Lakabu
      iii) Ngano za mtanziko

   b) i) Ngomezi ni nini? (alama 2)
      ii) Fafanua sifa nne za ngomezi. (alama 4)

   c) i) Eleza sifa nne za misimu. (alama 4)
      ii) Taja umuhimu nne za misimu. (alama 4)



**JINA**____________________ **NAMBARI YAKO**__________

**SHULE**____________________ **TAREHE** __________

**SAHIHI** __________

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**JULAI/AGOSTI 2015**
**FASIHI**
**Saa: 2 ½**

# MTIHANI WA MWIGO WA SHULE YA SEKONDARI ZA NAROK KUSINI

**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SEKONDARI KENYA (K.C.S.E.)**
**KISWAHILI**
**KARATASI 3**
**FASIHI**

**Maagizo**

a) Jibu Maswali **Manne** pekee
b) Swali la **Kwanza** ni la **lazima**
c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi au Fasihi simulizi
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

**Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

## SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1. SWALI LA LAZIMA

Soma shairi hili kisha ujibu maswaliyanayofuata:-

Hao miungu waliosimama kichaka
Wambieni wakae chini warefu.
Kaeni chini Wengi nyuma, hatuoni!
Hatutaki vyenu vichafu visogo kuona
Kaeni chini miungu, kaeni chini.

Ndugu kaeni chini, kaeni chini ndiyo amri
Acheni kelele, kelele za jaza - tumbo
Kaeni tulo nyuma kweli yatuchoma mioyo
Twataka kuchagau watu watu watu
Mlipewa uongozi, ukawapaka rangi
Na madaraka, madaraka yakawalevya
Sasa yavueni wapisheni wenye nia!

Ama hamjaona hasira, ikifura ya wengi watu?
Ulizeni ya Saidi aliyechomoa sokoni
Na ya Abdalla aliyegonga masikini?
Miungu, nanyi ndugu, chini pwetekeni
Tuwakanyage tupitie mbele tujisukume
Sisi twauza bidhaa ninyi mwauza maneno!
Tuko sawa haikai mdomoni.

Kataeni yote misituni, fimbo tuenee
Na vivyago tuwachonge watoto wachezee
Kausheni yote maziwa maji tulowanishe
Kukipambazuka wasiweze ruka angani
Kokeni moto, mashujaa wa uonevu tuwabanike
Kamwe hapatakuwa na kilio wala matanga
Bali hoi hoi ushindi na madaraka kwa umma.



Maswali

a) Andika mambo manne anayolalamikia mshairi? (alama 4)

b) Taja mambo matatu yanayodhihirisha kuwa hili ni shairi huru. (alama 3)

c) Mshairi ametumia inkisari. Thibitisha. (alama 2)

d) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)

e) Ukirejelea shairi hili, tolea mbinu hizi mfano mmoja mmoja. (alama 4)
   - i) Nahau
   - ii) Jazanda
   - iii) Takriri
   - iv) Nidaa

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kwenye shairi. (alama 3)
   - i) Wapisheni
   - ii) Pwetekeni
   - iii) Tuwabanike

## SHEEMU YA B: TAMTHILIA

**Jibu swali la 2 au la 3**

Timothy M. Arege: Mstahiki Meya

2. "Uongozi unaotafuta dini utadumu maana umebarikiwa"
   - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   - b) Ni tamathali ipi ya usemi inayodhihirika katika dondoo hili? (alama 4)
   - c) Onyesha mifano mingine miwili ya tamathali uliyotaja tamthiliani. (alama 6)
   - d) Fafanua dhima ya msemaji katika tamthilia. (alama 6)

3. 
   - a) Onyesha athari za uongozi mbaya katika tamthilia. (alama 10)
   - b) Jadili mbinu ambazo wanacheneo walitumia kusuluhisha matatizo yaliyowakumba. (alama 10)